**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA**

# RIPOTI YA SITA

# YA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA TUME YA MAADILI KWA MWAKA 2021/2022

**Septemba, 2022**

**(Imewasilishwa kwa mujibu wa kifungu cha 29 cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Nam. 4 ya 2015)**

**YALIYOMO**

YALIYOMO........................................................................ i
**JADWELI, MICHORO NA VIAMBATANISHO.................. ii**
**MAELEZO YA MWENYEKITI ........................................ v**
1.0 UTANGULIZI.................................................................. 1
1.1 TUME YA MAADILI ....................................................... 1
1.2 DIRA............................................................................... 2
1.3 DHAMIRA ....................................................................... 2
1.4 MAADILI YA MSINGI ..................................................... 2
1.5 MALENGO YA TUME YA MAADILI............................... 3
**2.0 MAJUKUMU YA TUME YA MAADILI ........................ 3**
2.1 MAMLAKA NA UWEZO WA TUME YA MAADILI ..........4
**3.0 VIONGOZI WANAOSIMAMIWA NA TUME YA MAADILI .............................................................5**
**4.0 KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA 2021/2022 ...............................................6**
**5.0 UTEKELEZAJI WA KAZI ZILIZOPANGWA MWAKA 2021/2022 ...............................................7**
5.1 UPOKEAJI NA USAJILI WA TAARIFA ZA MALI NA MADENI YA VIONGOZI WA UMMA...................................8
5.1.1 Tamko la Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma .....8
5.1.2 Uchapishaji na Usambazaji wa Fomu ya Tamko la Mali na Madeni..........................................................8
5.1.3 Uchambuzi wa Fomu ...............................................8
5.2 UHAKIKI WA TAARIFA ZA MALI NA MADENI YA VIONGOZI WA UMMA.....................................................12
5.2.1 Uchambuzi wa Taarifa za Uhakiki ..........................12
5.3 MFUMO WA KIELEKTRONIKI WA USAJILI WA TAARIFA ZA MALI NA MADENI YA VIONGOZI WA UMMA.14
5.4 UPOKEAJI NA UCHUNGUZI WA TUHUMA NA MALALAMIKO YA UKIUKWAJI WA SHERIA YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA ................................16
5.4.1 Uchambuzi wa Malalamiko ...................................17

5.5 KUJENGA UELEWA KWA WANANCHI NA VIONGOZI WA UMMA UNGUJA NA PEMBA KUHUSU MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA....................................18
5.5.1 Mikutano na Viongozi wa Umma na Wananchi........19
5.5.2 Utayarishaji na Urushaji wa Vipindi vya Elimu na Matangazo kupitia Vyombo vya Habari .......................21
5.5.3 Utayarishaji na Utoaji wa Matangazo ......................21
5.5.4 Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu .........................................................................22
5.6 MAFUNZO YA KITAALAM KWA WATUMISHI WA TUME YA MAADILI ......................................................23
5.7 KUANDAA NA KUWASILISHA RIPOTI YA MWAKA YA KAZI ZA TUME YA MAADILI..........................................23
**6.0 VIKAO VYA TUME YA MAADILI ............................24**
6.1 KUSIKILIZA NA KUTOA MAAMUZI KUHUSU MALALAMIKO YA UVUNJAJI WA MAADILI YA VIONGOZI 24
**7.0 HALI YA MAPATO NA MATUMIZI ..........................25**
**8.0 CHANGAMOTO NA UTATUZI WAKE ......................26**
**9.0 MIKAKATI YA TUME YA MAADILI KWA MWAKA 2022/2023 ...............................................27**
**10.0 HITIMISHO ...........................................................28**
**11.0 UWASILISHAJI WA RIPOTI .................................28**

## JADWELI, MICHORO NA VIAMBATANISHO

### JADWELI

Jadweli Nambari 1: Taarifa za Watumishi wa Tume ya Maadili na Viwango vyao vya Elimu. ...............................2

Jadweli Nambari 2: Muhtasari wa Uwasilishaji wa Fomu .10

Jadweli Nambari 3: Viongozi Waliochelewa Kuwasilisha Fomu ya Tamko kwa 2021/2022 ..................................11

Jadweli Nambari 4: Uhakiki kwa Viongozi wa Umma kwa mwaka 2021/2022 ..................................................13

Jadweli Nambari 5: Idadi ya Malalamiko iliyopokelewa 2021/2022. ..............................................17

Jadweli Nambari 6: Uchambuzi wa Malalamiko iliyopokelewa kwa 2021/2022. .......................................18

Jadweli Nambari 7: Orodha ya Shehia na Wananchi wake Zilizopatiwa Elimu ya Maadili. ...............................20

Jadweli Nambari 8: Orodha ya Skuli na Wanafunzi Zilizopatiwa Elimu ya Maadili. .......................................20

Jadweli Nambari 9: Orodha ya Mabaraza na Vijana Yaliyopatiwa Elimu ya Maadili. ............................21

Jadweli Nambari 10: Hali ya Mapato na Matumizi...........26

### MICHORO

Mchoro Nambari 1: Viongozi Waliochelewa Kuwasilisha Fomu. ...................................................................10

Mchoro Nambari 2: Uhakiki kwa Viongozi wa Umma
kwa mwaka 2020/2021 ................................................13

**VIAMBATANISHO**

Kiambatanisho Nambari 1: Muundo wa Tume ya Maadili
ya Viongozi wa Umma....................................................30

## MAELEZO YA MWENYEKITI

Kifungu cha 29 cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Nam. 4 ya 2015, kinamuelekeza Mwenyekiti wa Tume ya Maadili ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya mwisho wa mwaka wa fedha kumalizika kutayarisha Ripoti ya Mwaka ya Utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili na kuiwasilisha kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Aidha, sheria imempa mamlaka Rais wa Zanzibar kumtaka Waziri anayehusika na masuala ya Maadili kuiwasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi katika kikao kinachofuata.

Ripoti hii ya Sita ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imetayarishwa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa ajili ya kuwasilishwa kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na hatimaye mbele ya Baraza la Wawakilishi.

Tume ya Maadili imeanzishwa kwa lengo la kuimarisha utawala bora nchini. Tume ya Maadili imepewa jukumu la kuhakikisha kuwa viongozi wa umma wanafuata masharti ya Sheria ya Maadili inayowataka kujaza Fomu ya Tamko la Mali na Madeni na kubainisha mali na madeni yao pamoja na mali na madeni ya wake, waume na watoto wao walio chini ya umri wa miaka 18. Taarifa hizo hupokelewa, kusajili na kufanyiwa uhakiki ili kuthibitisha usahihi wake.

Katika kuhakikisha viongozi wa umma wanafuata masharti ya Sheria ya Maadili, Tume imepewa jukumu la kupokea kutoka kwa wananchi malalamiko au tuhuma za ukiukwaji wa maadili dhidi ya Viongozi wa Umma na kufanya uchunguzi kuhusu tuhuma au malalamiko hayo. Kadhalika, Tume inatakiwa kuwaelimisha viongozi wa umma na wananchi kuhusu umuhimu wa kuzingatia na kufuata maadili katika

utekelezaji wa majukumu yao kwa umma. Hivyo, Ninapenda kuchukua fursa hii kuelezea kwa ufupi tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Maadili katika kipindi mwaka wa fedha 2021/2022.

Katika mwaka 2021/2022 jumla ya viongozi 2,496 waliwasilisha Fomu za Tamko la Mali na Madeni sawa na asilimia 99.8 ya shabaha iliyopangwa. Orodha ya Majina ya Viongozi wa Umma waliowasilisha Fomu za Tamko la Mali na Madeni ilichapishwa katika Gazeti la Serikali kupitia Tangazo la Kisheria Nambari 39 na 101 la Mwaka 2022. Orodha hii imetumika na kusaidia kubaini viongozi waliowasilisha nje ya muda uliowekwa kisheria na wale walioshindwa kuwasilisha Fomu ***Jadweli Nambari 2 na 3 yanahusika.***

Katika kipindi hiki cha utekelezaji 2021/2022, idadi ya viongozi waliofanyiwa uhakiki iliongezeka na kufikia 224 sawa na asilimia 112 ya lengo la kuhakiki viongozi 200. Idadi hiyo iliongezeka ukilinganisha na mwaka uliopita 2020/2021 ya viongozi 207. ***Jadweli Nambari 4 linahusika.***

Katika kipindi hiki cha utekelezaji, Tume imeendelea kuimarisha Mfumo wa Kieletroniki wa Usajili wa Taarifa za Mali na Madeni ya Viongozi kwa kupokea Fomu za viongozi kwa kutumia mfumo wa kielektroniki, kutoa barua ya kupokelewa Fomu kwa njia ya kielektroniki na taarifa ya ujumbe kupitia simu ya kiongozi husika kujuulishwa kuwa fomu yake imepokelewa na Tume. Kwa kiwango kikubwa na cha kuridhisha, mfumo huo umerahisisha sana kazi ya upokeaji Fomu na uchapishaji wa orodha ya Viongozi wa Umma katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Kwa upande wa malalamiko yanayohusiana na uvunjwaji wa maadili kutoka kwa wananchi, jumla ya malalamiko 22

yamepokelewa na kufanyiwa kazi sawa na asilimia 110 ya shabaha iliyokadiriwa. Maeneo ambayo malalamiko hayo yalijikita ni pamoja na matumizi mabaya ya madaraka (18), udhalilishaji wa kijinsia (2), upendeleo katika ajira (1) na kutelekeza familia (1). Malalamiko hayo yako katika hatua tofauti za kufanyiwa kazi ***Jadweli Nambari 5 na 6 yanahusika.*** Malalamiko hayo yaliwahusu viongozi na watendaji wakuu wa Wizara, Idara na Taasisi za SMZ wakiwemo baadhi ya Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, Wilaya na Masheha. Aidha, ripoti ya uamuzi uliotolewa na Tume kuhusiana na malalamiko yaliyokamilika tayari imewasilishwa kwenye mamlaka husika za kinidhamu kwa ajili ya hatua za utekelezaji.

Katika kuongeza uelewa juu ya dhana nzima ya umuhimu wa maadili kwa Viongozi wa Umma na jamii, Tume ilirusha hewani vipindi 12 vya utoaji elimu kupitia redio na televisheni. Kadhalika, Tume ilifanya mikutano 75 ya utoaji elimu ikishirikisha viongozi, wananchi, wanafunzi, vijana na wasanii.

Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu yalifanyika tarehe 13 Disemba, 2021 ambapo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi alikuwa mgeni rasmi. Maadhimisho hayo yaliandaliwa kwa ushirikiano kati ya taasisi zote zinazohusika na masuala ya Utawala Bora. Taasisi hizo ni Tume ya Maadili, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Idara ya Utawala Bora na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Katika kipindi hiki cha utekelezaji, tarehe 19 Januari, 2022 Tume ya Maadili ilipata msiba wa kuondokewa na

Kamishana Said Bakari Jecha. Marehemu Said Bakar Jecha ni miongoni mwa Makamishna waanzilishaji wa Tume ya Maadili. Marehemu alijitolea kwa moyo wake wote katika kutekeleza majukumu yake akiwa Kamishana wa Tume ya Maadili. Hivyo, ninachukua fursa hii kutoa pole kwa familia na ndugu wa Marehemu Said Bakari Jecha kutokana na kifo chake. Mchango wake katika kuimarisha utawala bora na ujenzi wa taifa letu unathaminiwa na daima utakumbukwa.

Kadhalika, katika kipindi hiki cha utekelezaji, Kamishna Sebtuu Mohamed Nassor amemaliza muda wake wa kipindi cha Pili cha kuitumikia Tume katika nafasi yake ya Kamishna. Mhe. Sebtuu naye ni miongoni mwa Makamishna wa mwanzo wa Tume. Katika hatua za kuhakikisha kazi za Tume hazisimami, Tume imepata Makamishna wapya wawili, Mhe. Balozi Mohammed Mwinyi Mzale na Mhe. Dkt. Maua Abeid Daftari.

Mafanikio kadhaa yamepatikana katika utekelezaji wa kazi za Tume. Mafanikio hayo yamechangiwa na Uongozi imara wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi.

Hivyo basi, ninaomba kutoa shukrani zangu za dhati na kipekee kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Shukrani hizo zinatokana na jitihada zake za kuimarisha Utawala Bora nchini katika maeneo ya uwazi, uwajibikaji na kuimarisha maadili kupitia Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma pamoja na taasisi nyengine za Umma na Utawala Bora.

Pili, ninawashukuru Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili wa Rais, Mhe.

Hemed Suleiman Abdalla, kwa kuendelea kumshauri vyema Mhe. Rais wa Zanzibar pamoja na kusimamia utendaji wa shughuli za Serikali katika mambo mbalimbali ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Tatu, namshukuru kwa dhati Waziri wa Nchi (AR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mhe. Mwalim Haroun Ali Suleiman, pamoja na viongozi wote wa Wizara kwa mwongozo, ushauri na msaada waliotupatia katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Maadili.

Nne, ninawashukuru Makamishna wa Tume ya Maadili, Mhe. Balozi Mohammed Mwinyi Mzale, Mhe. Sebtuu Mohammed Nassor ambaye amemaliza vipindi viwili vya utumishi wake Julai, 2022 pamoja na Kamishna mpya Mhe. Dkt. Maua Abeid Daftari.

Vilevile, namshukuru Katibu wa Tume ya Maadili, Nd. Asma Hamid Jidawy pamoja na watendaji wote wa Tume ya Maadili kutokana na utendaji wao uliotuwezesha kupata mafanikio tuliyoyafikia katika kipindi hiki cha utekelezaji. Ninaendelea kutoa wito kwa Viongozi wa Umma na Wananchi wote waendelee kutoa ushirikiano ambao utaiwezesha Tume ya Maadili kutekeleza majukumu yake kikamilifu ili hatimaye kufikia lengo la kuimarisha Utawala Bora katika nchi yetu.

Kwa heshima, naomba kuwasilisha.



**Assaa Ahmad Rashid**
**Mwenyekiti**
**Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

***'Fuata Maadili, Tuimarishe Utawala Bora'.***

## 1.0 UTANGULIZI

Ripoti hii ya Sita ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili inaelezea kazi za Tume kwa mwaka 2021/2022 uliofanywa kwa kuzingatia Mpangokazi wa Tume ya Maadili wa mwaka 2021/2022, Mipango Mikuu ya Kitaifa ikijumuisha Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020-2025.

### 1.1 TUME YA MAADILI

Tume ya Maadili imeanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya 2015 na inaundwa na Mwenyekiti na Makamishna wawili wanaoteuliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mwenyekiti anasimamia majukumu na mamlaka ya Tume kuhusiana na masuala ya maadili. Katibu wa Tume, ambaye pia anateuliwa na Rais wa Zanzibar chini ya kifungu cha 10A(1) cha Sheria, anasimamia kazi za kiutawala za kila siku na anawajibika kwa Tume.

Kwa upande wa Pemba, Afisi ya Tume ya Maadili inasimamiwa na Afisa Mdhamini anayeratibu shughuli za Tume ya Maadili Pemba. Tume, pia, ina watumishi wa fani mbalimbali ikiwemo Sheria, Mipango, Utunzaji wa kumbukumbu, Utumishi, Utawala, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Uhusiano na Elimu kwa Umma, Ualimu, Ununuzi, fedha na Uhasibu. Muundo wa Tume ya Maadili na Taarifa za Watumishi na elimu zao ni kama inavyoonekana katika ***Jadweli Nambari 1*** na ***Kiambatanisho Nambari 1.***

**Jadweli Nambari 1: Taarifa za Watumishi wa Tume ya Maadili**

| FORM II-VI/CHETI | | STASHAHADA | | STASHA HADA YA JUU | | SHAHAD A | | STASHAH ADA YA UZAMILI | | SHAHADA YA UZAMILI | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| KE | ME | KE | ME | KE | ME | KE | ME | KE | ME | KE | ME | |
| 1 | 5 | 3 | - | 0 | 0 | 5 | 2 | 0 | 1 | 4 | 5 | **26** |

## 1.2 DIRA

Dira ya Tume ya Maadili ni *"Kuwa na jamii yenye kufuata maadili"*

## 1.3 DHAMIRA

Dhamira ya Tume ya Maadili ni "Kukuza tabia na vitendo vyenye kufuata maadili kwa Viongozi wa Umma kwa kuimarisha uwazi, uwajibikaji, utii na usimamizi wa sheria".

## 1.4 MAADILI YA MSINGI

Utendaji kazi wa Tume ya Maadili umejengwa kwa kuzingatia misingi ya maadili ifuatayo ambayo inawaongoza watumishi wake:

(a) Uadilifu: Kufanya kazi kwa uwazi na bila ya upendeleo;
(b) Usiri: kuhifadhi na kutunza taarifa zote za siri ikiwemo taarifa zinazohusiana na mali na madeni ya Viongozi wa Umma;
(c) Utaalamu: Kusimamia sheria ya Maadili ya Viongozi kwa umakini na uaminifu kwa kutumia umahiri, uweledi, na utaalamu unaohitajika;
(d) Uwajibikaji: Kuimarisha uwajibikaji wa watumishi na wahusika wengine wa Tume; na
(e) Kufanya kazi kwa mashirikiano: Kukuza na kuimarisha ushirikiano miongoni mwa watumishi ili kuwezesha utendaji wa kazi za Tume kwa ufanisi.

## 1.5 MALENGO YA TUME YA MAADILI

Lengo kuu la Tume ya Maadili ni "Kusimamia Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar". Malengo mahsusi ya Tume ni pamoja na:-

i. Kuimarisha Usajili wa Taarifa za Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma;
ii. Kuimarisha uhakiki wa Taarifa za Mali na Madeni kwa Viongozi wa Umma;
iii. Kuimarisha uchunguzi wa malalamiko, madai na tuhuma za uvunjaji wa maadili dhidi ya Viongozi wa Umma;
iv. Kujenga uelewa kwa Wananchi na Viongozi wa Umma kuhusu umuhimu wa Maadili;
v. Kuimarisha uwezo wa Tume ya Maadili kiutendaji.

## 2.0 MAJUKUMU YA TUME YA MAADILI

Majukumu ya Tume ya Maadili yanabainishwa katika kifungu cha 12(1) cha Sheria ya Maadili kama ifuatavyo:

(a) Kupokea na kuhifadhi Tamko la Mali na Madeni ambalo limetolewa na Kiongozi wa Umma;
(b) Kupokea tuhuma na taarifa za uvunjaji wa maadili kutoka kwa wananchi;
(c) Kufanya uchunguzi juu ya madai au tuhuma za uvunjaji wa maadili kwa kiongozi yeyote wa Umma;
(d) Kupokea, kuchunguza na kushughulikia madai yote yanayohusu uvunjaji wa maadili katika chombo cha umma;
(e) Kupokea na kuchunguza jambo lolote ambalo kwa maoni ya Tume linapelekea tuhuma ya moja ya mambo yafuatayo kuwa limetokea au linaweza kutokea:
(i) Kitendo kinachopelekea uvunjaji wa maadili;
(ii) Kitendo kinachopelekea kuruhusu, kushawishi au

kusababisha uvunjaji wa maadili;

(f) Kuchunguza mwenendo wa kiongozi yeyote wa umma ambao kwa maoni ya Tume, unapelekea au unachangia uvunjaji wa maadili;

(g) Kusikiliza na kutoa maamuzi kuhusu madai yoyote ya uvunjaji wa Maadili dhidi ya Kiongozi wa Umma;

(h) Kutoa uamuzi wa uvunjaji wowote wa maadili;

(i) Kusaidia taasisi yoyote ya Serikali yenye jukumu la kutekeleza Sheria katika kufanya uchunguzi wa kosa la uvunjaji wa maadili;

(j) Kutokana na maombi ya mtu au taasisi yoyote, kushauri au kusaidia mtu au taasisi yoyote namna ambavyo kiongozi au taasisi hiyo inavyoweza kuepukana na uvunjaji wa maadili;

(k) Kuelimisha umma juu ya umuhimu wa maadili;

(l) Kufanya uchunguzi juu ya jambo lolote ambalo kwa maoni ya Tume linastahili kufanyiwa uchunguzi;

(m) Kutoa ushauri, maelekezo na miongozo kuhusiana na maadili ya Viongozi;

(n) Kufanya uhakiki wa moja kwa moja kuhusiana na Tamko la Mali na Madeni lililowasilishwa kwa mujibu wa sheria; na

(o) Kufanya kazi nyengine zozote ilizopewa na Sheria ya Maadili ya Viongozi au Sheria nyenginezo.

## 2.1 MAMLAKA NA UWEZO WA TUME YA MAADILI

Katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake, Tume ya Maadili imepewa mamlaka na uwezo wa:-

.

(a) Kumuidhinisha Afisa wa Tume kufanya uchunguzi wa tuhuma ya uvunjaji wa maadili (kif. 13(1)(a)).

(b) Kumtaka mtu yeyote kutoa kumbukumbu na nyaraka zozote zinazohusiana na tuhuma zinazofanyiwa uchunguzi (kif. 13(1)(b)).

(c) Kumtaka mtu yeyote kufika mbele ya Tume kwa ajili ya kuhojiwa kuhusiana na jambo lolote linaloshughulikiwa na Tume katika uchunguzi wa tuhuma za uvunjaji wa maadili (kif.13(1)(c)).
(d) Kumtaka Kiongozi wa Umma kutoa taarifa au maelezo ya ziada kuhusiana na Tamko la Mali na Madeni alililoliwasilisha (kif.16A).
(e) Kushirikiana na taasisi au mtu yeyote katika uchunguzi wa madai au tuhuma za uvunjaji wa Sheria ya Maadili (kif. 14(1)).
(f) Kuchunguza Akaunti ya Kiongozi wa Umma (kif.37(1)).
(g) Kuwasilisha maamuzi yake kwenye mamlaka husika (kif. 27(1)).

## 3.0 VIONGOZI WANAOSIMAMIWA NA TUME YA MAADILI

Kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, viongozi wanaosimamiwa na kuwajibika na masharti ya Sheria hiyo wamegawanyika katika makundi makuu kama ifuatavyo:

**i) Viongozi wanaochaguliwa na wananchi**

Kundi hili linajumuisha Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani.

**ii) Viongozi wanaoteuliwa na Rais wa Zanzibar**

Kundi hili linajumuisha Makamo wa Kwanza wa Rais, Makamo wa Pili wa Rais, Jaji Mkuu, Kadhi Mkuu, Mufti, Mawaziri, Washauri, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Wakurugenzi, Mameneja, Wakuu wa Idara Maalum, Taasisi, Mashirika, Tume, Kamisheni, Wakala, Idara, Wenyeviti wa Bodi, n.k.

**iii) Viongozi wanaoteuliwa na Waziri**

Kundi hili linajumuisha Warajis, Maafisa, Wajumbe wa Bodi, Baraza, Mashirika, Wakala, n.k.

**iv) Viongozi Wanaoteuliwa na Bodi**

Kundi hili linajumuisha viongozi wanaoteuliwa na Bodi ya Wakurugenzi au Ushauri za Mashirika, Kamisheni, Wakala, Tume na taasisi nyengine za Umma kama vile Katibu wa Bodi, Mameneja, Wakurugenzi, Maafisa Dhamana, Wakuu wa Vitengo na Sehemu, n.k.

**v) Viongozi walioainishwa kutokana na Unyeti na Uzito wa Kazi na Majukumu yao**

Kundi hili linajumuisha Mahakimu, Wahasibu, Wakaguzi wa Hesabu za Serikali, Maafisa Kodi na Mapato, n.k.

Kwa mujibu wa Sheria hiyo, Viongozi hao wanawajibika kufuata masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi. Miongoni mwa masharti hayo ni kujaza na kuwasilisha Tume ya Maadili, Fomu ya Tamko la Mali na Madeni ndani ya muda uliowekwa kisheria. Aidha, Sheria inawataka viongozi hao, katika utekelezaji wa majukumu yao, kufuata maadili na miiko ya uongozi iliyobainishwa katika Sheria ya Maadili ya Viongozi na Sheria nyengine za nchi. Orodha ya Viongozi wanaowajibika na Masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni kama inavyoonekana katika ***Kiambatanisho Nambari 2.***

## 4.0 KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA 2021/2022

Kwa mwaka 2021/2022 Kazi zifuatazo zilipangwa kutekelezwa:-

(a) Kupokea na kusajili Taarifa za Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma;

(b) Kufanya uhakiki wa Taarifa za Mali na Madeni kwa Viongozi wa Umma pamoja na kuandaa taarifa ya uhakiki;

(c) Kuimarisha Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili wa Taarifa za Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma;

(d) Kupokea, kufanya uchunguzi na kusikiliza malalamiko na tuhuma za uvunjwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(e) Kujenga uelewa kwa Viongozi wa Umma na Wananchi Unguja na Pemba kuhusu umuhimu wa Maadili ya Viongozi wa Umma;

(f) Kuadhimisha siku ya Maadili na Haki za Binadamu duniani;

(g) Kuwapatia mafunzo ya kitaalam Watumishi wa Tume ya Maadili; na

(h) Kuandaa na kuwasilisha Ripoti ya Mwaka ya Kazi za Tume.

## 5.0 UTEKELEZAJI WA KAZI ZILIZOPANGWA MWAKA 2021/2022

Katika kipindi hiki cha utekelezaji, Tume ya Maadili imetekeleza kazi zake kama ifuatavyo:-

## 5.1 UPOKEAJI NA USAJILI WA TAARIFA ZA MALI NA MADENI YA VIONGOZI WA UMMA

### 5.1.1 Tamko la Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma

Kifungu cha 15 cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kimeweka utaratibu wa uwasilishaji wa Fomu ya Tamko la Mali na Madeni kwa kila kiongozi wa umma aliyetajwa katika Jadweli la Kwanza la Sheria ya Maadili kwa utaratibu ufuatao:

(a) kila ifikapo mwezi wa Disemba ya kila mwaka,
(b) ndani ya siku thelathini (30) baada ya kiongozi wa umma kushika madaraka au wadhifa wa uongozi; na
(c) mara tu baada ya kiongozi wa umma kumaliza muda wa kushika madaraka au wadhifa wa uongozi.

### 5.1.2 Uchapishaji na Usambazaji wa Fomu ya Tamko la Mali na Madeni

Katika mwaka wa fedha 2021/2022, fomu 6,000 za Tamko la Mali na Madeni zilichapishwa na kusambazwa kwa viongozi katika makao makuu ya kila Wizara na taasisi zote zinazojitegemea. Kadhalika, fomu hizo zilipatikana katika Ofisi za Tume ya Maadili Vuga, Unguja na Chake Chake, Pemba pamoja na kwenye tovuti ya Tume ya Maadili **"www.ethicscommission.go.tz".** Tume imeendelea kuwahimiza viongozi kuendelea kutumia njia ya kupata fomu kupitia tovuti ya Tume ya Maadili ili kupunguza gharama za uchapishaji na usambazaji.

### 5.1.3 Uchambuzi wa Fomu

Kwa mwaka 2021/2022 jumla ya Fomu 2,500 zilikadiriwa kupokewa ambapo Fomu 2,381 zilipokelewa hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2021 sawa na asilimia 95 ya makadirio yaliyopangwa (fomu zilizopokelewa Unguja 1,994 na Pemba

387). Hata hivyo, Fomu ziliendelea kupokewa kutoka kwa viongozi waliochelewa na waliopata uteuzi mpya baada ya tarehe 31 Disemba 2021. Hivyo, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 Fomu 2,496 zilipokelewa sawa na asilimia 99.8 ya lengo lililowekwa katika Mpango Kazi wa mwaka 2021/2022. Kati ya Fomu 2,496, Fomu zilizowasilishwa ndani ya muda ni 2,485 na zilizowasilishwa nje ya muda ni 11. Ukilinganisha na mwaka uliopita 2020/2021, kumekuwa na upungufu wa idadi ya viongozi wanaochelewa kurejesha Fomu. Hali hii inaashiria kuwa urejeshaji wa fomu kwa wakati uliowekwa kisheria umetokana na mwamko walionao viongozi kutokana na elimu inayoendelea kutolewa na Tume ya Maadili.


Kwa kuwa kuchelewa kurejesha Fomu kwa wakati bila ya sababu za msingi ni kosa la kimaadili, viongozi waliochelewa kurejesha Fomu kwa wakati waliitwa mbele ya Tume na kupewa fursa ya kutoa maelezo na sababu za kuchelewa kwao. Tume ilifanya maamuzi ambapo uamuzi kuhusu viongozi ambao sababu zao zilionekana kuwa sio za msingi, uliwasilishwa kwenye mamlaka zao za uteuzi kwa hatua za kinidhamu. Kwa ujumla kazi ya upokeaji na usajili wa Fomu kwa mwaka 2021/2022 imefanyika kwa mafaniko na ufanisi zaidi.

Muhtasari wa uwasilishaji wa fomu ni kama unavyoonekana katika ***Jadweli Nambari 2 na Mchoro Nambari 1.*** Aidha, Mchanganuo wa Viongozi waliochelewa kuwasilisha Fomu ni kama unavyoonekana katika ***Jadweli Nambari 3.***

## Jadweli Nambari 2: Muhtasari wa Uwasilishaji wa Fomu

| MAELEZO | 2017/2018 | 2018/2019 | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| MAKADIRIO | 1,650 | 1,650 | 2,500 | 2,500 | 2,500 |
| FOMU ZILIZOWASILISHWA | 1,664 | 1,702 | 2,325 | 2,578 | 2,496 |
| ZIADA/(UPUNGUFU) | 14 | 52 | (172) | 78 | (4) |
| ASILIMIA - UWASILISHAJI | 101 | 103 | 93 | 103 | 99.8 |
| NDANI YA MUDA | 1,639 | 1,676 | 2,245 | 2,526 | 2,485 |
| WALIOCHELEWA | 25 | 26 | 53 | 52 | 11 |
| ASILIMIA - WALIOCHELEWA | 2 | 2 | 2 | 2 | 0.4 |

## Mchoro Nambari 1: Muhtasari wa Uwasilishaji wa Fomu



**Jadweli Nambari 3: Viongozi Waliochelewa kuwasilisha Fomu ya Tamko 2021/2022**

| NAM | MAELEZO | IDADI | HATUA |
|---|---|---|---|
| 1 | Viongozi wanaochaguliwa na Wananchi | 1 | Viongozi walipewa fursa ya kutoa sababu na maelezo ya kuchelewa kuwasilisha Fomu kwa wakati.<br><br>Viongozi ambao sababu zao zilionekana kuwa sio za msingi, uamuzi wa Tume uliwasilishwa kwenye mamlaka zao za uteuzi kwa hatua za kinidhamu. |
| 2 | Viongozi wanaoteuliwa na Rais wa Zanzibar | 5 | |
| 3 | Viongozi wanaoteuliwa na Waziri | 2 | |
| 4 | Viongozi wanaoteuliwa na Bodi | 2 | |
| 5 | Viongozi walioainishwa kutokana na unyeti na uzito wa kazi na majukumu yao | 1 | |
| | **Jumla** | **11** | |

**Mchoro Nambari 1: Viongozi Waliochelewa kuwasilisha Fomu**



### 5.1.4 Kutangaza Majina ya Viongozi wa Umma katika Gazeti Rasmi la Serikali

Kifungu cha 22(3) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, kinaelekeza kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali Majina ya Viongozi wa Umma waliowasilisha Fomu. Kwa mwaka 2021/2022 Majina ya Viongozi wa Umma waliowasilisha Fomu yamechapishwa katika Tangazo la Kisheria Nambari 39 na 101 la mwaka 2022. Orodha ya Kwanza ya majina inajumuisha Viongozi wa Umma waliowasilisha Fomu zao hadi mwezi Januari, 2022. Orodha ya Pili ni ya viongozi walioteuliwa baada ya mwezi Januari, 2022 hadi mwezi Juni, 2022.

## 5.2 UHAKIKI WA TAARIFA ZA MALI NA MADENI YA VIONGOZI WA UMMA

Kifungu cha 12(1)(n) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kimeweka utaratibu wa Uhakiki wa Taarifa za Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma. Kwa mujibu wa kifungu hicho, Tume inaweza kufanya uhakiki wa taarifa zilizomo kwenye Fomu ya Tamko la Mali na Madeni kwa lengo kuhakikisha usahihi wa taarifa hizo.

### 5.2.1 Uchambuzi wa Taarifa za Uhakiki

Jumla ya Viongozi 224 wamefanyiwa uhakiki Unguja na Pemba katika mwaka huu wa utekelezaji 2021/2022. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 112 ya shabaha ya Viongozi 200 waliopangwa kuhakikiwa. Kumekuwa na ongezeko la viongozi 17 ikilinganishwa na viongozi 207 waliohakikiwa katika mwaka 2020/2021. Muhtasari wa ulinganisho wa uhakiki kwa viongozi wa umma ni kama unavyoonekana katika ***Jadweli Nambari 4 na Mchoro Nambari 2.***


## Jadweli Nambari 4: Uhakiki kwa Viongozi wa Umma hadi mwaka 2021/2022

**Jadweli Nambari 4: Uhakiki kwa Viongozi wa Umma hadi mwaka 2021/2022**

| MWAKA | VIONGOZI WALIOPANGWA KUHAKIKIWA | UTEKELEZAJI HALISI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| 2016/2017 | 56 | 38 | 68 |
| 2017/2018 | 360 | 103 | 29 |
| 2018/2019 | 120 | 168 | 140 |
| 2019/2020 | 220 | 135 | 61 |
| 2020/2021 | 200 | 207 | 104 |
| 2021/2022 | 200 | 224 | 112 |

## Mchoro Nambari 2: Uhakiki kwa Viongozi wa Umma kwa mwaka 2021/2022

**Mchoro Nambari 2: Uhakiki kwa Viongozi wa Umma kwa mwaka 2021/2022**




Kazi ya uhakiki kwa mwaka 2021/2022 ilihusisha Mawaziri, Makatibu na Manaibu Katibu Wakuu, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Makamishna, Wakuu wa Wilaya, Maafisa Wadhamini, Makatibu wa Rais, Wasaidizi wa Rais na Makamu wa Rais wa Kwanza na Pili, Katibu Mtendaji,

Wakurugenzi, Wakurugenzi Watendaji na Waendeshaji, Wakurugenzi Wakuu, Wakuu wa Vikosi, Maafisa wa Baraza la Mapinduzi, Makamu Mkuu wa Chuo, Jaji, Mahakimu, Makadhi, Mwenyekiti, Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu, Mameneja, Maafisa Kodi na Mapato.

Kukosekana kwa nyaraka za umiliki wa mali zilizoorodheshwa kwenye Fomu za Tamko la Mali na Madeni limeendelea kuwa ni tatizo kubwa. Viongozi wengi wameorodhesha mali ambazo hawajakamilisha taratibu za uhaulishaji wa mali hizo. Wito unatolewa kwa viongozi kukamilisha taratibu za uhaulishaji wa mali zao ili kurahisisha uwekaji wa kumbukumbu sahihi za taarifa na mali zao katika Daftari la Usajili wa Taarifa za Mali na Madeni za Viongozi wa Umma.

## 5.3 MFUMO WA KIELEKTRONIKI WA USAJILI WA TAARIFA ZA MALI NA MADENI YA VIONGOZI WA UMMA

Katika kipindi hiki cha utekelezaji, Tume imeendelea kuimarisha Mfumo wa Kieletroniki wa Usajili wa Taarifa za Mali na Madeni kwa kupokea Fomu za viongozi kwa kutumia mfumo wa kielektroniki, kupatiwa barua ya kupokelewa Fomu kwa njia ya kielektroniki na taarifa ya ujumbe kupitia simu ya kiongozi husika kujuulishwa kuwa Fomu yake imepokelewa na Tume. Mfumo huo umerahisisha kazi ya upokeaji Fomu, kuhifadhi taarifa na uchapishaji wa orodha ya Viongozi wa Umma katika Gazeti Rasmi la Serikali. Kadhalika, Mfumo pia unatumika katika kupokea na kutunza taarifa za uhakiki wa mali za viongozi, zinazounganishwa na taarifa za mali zilizowasilishwa na viongozi katika Fomu zao.

Aidha, Mfumo huu utakapokamilika unatarajiwa kutoa taarifa za kumbukumbu za viongozi wanaofanyiwa uhakiki katika maeneo ya mali zao kupitia mfumo wa taarifa za kimaeneo (Geographical Information System) pamoja na kulinganisha

tamko halisi la Taarifa za Mali na Madeni lililotolewa na kiongozi husika na uhalisia wa Taarifa za Mali na Madeni za kiongozi baada ya kufanyika uhakiki.

Mfumo huu utawezesha Tume kuendesha shughuli zake za uhakiki kwa urahisi kabisa kupitia taarifa ambazo zitakuwa zinawasaidia Maofisa wa Tume kuyatambua maeneo waliokwisha kuyahakiki, na pia kupanga ratiba za uhakiki kikamilifu kulingana na taarifa za mali za viongozi na maeneo zinakopatikana mali hizo ili kuepusha usumbufu wa kurudia eneo moja mara kwa mara kuhakiki viongozi tofauti.

Kadhalika, Mfumo utawezesha wakuu wa Tume kutambua maeneo wanayohakiki Maofisa wa Tume kipindi cha uhakiki ili kusaidia kuongeza uwazi katika zoezi la uhakiki na kusaidia katika kutoa taarifa sahihi za uhakiki. Mfumo umewekewa uwezo wa kuchukua taarifa za kimaeneo kwa kila eneo ambalo Afisa atakuwa anachukuwa taarifa za uhakiki za mali za kiongozi na kuzituma kwenye mfumo ili kusaidia kujua eneo aliko Afisa na mali inayohakikiwa. Mfumo utakua na uwezo wa kulinganisha mali zilizomo kwenye mfumo na zile zilizotumwa ili kutoa taarifa muhimu.

Katika juhudi za kuimarisha ubadilishanaji wa taarifa kwa taasisi za serikali, Mfumo wa Tume utaweza kuunganishwa na mifumo mengine yenye taarifa zinazohitajika na Tume kwa lengo la kupata na kujua taarifa nyengine za viongozi. Mfano wa mifumo itayoweza kuunganishwa ni Mfumo wa Watumishi wa Umma (Human Resource Information System) na Mfumo wa Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi (Zan ID System). Hatua hiyo itarahisisha kazi ya kupata takwimu na taarifa sahihi za viongozi. Hata hivyo, kutokana na usiri wa taarifa zitakazokua katika mfumo huu, mfumo kwa sasa hautakua na taarifa za kutoa kwenda katika mifumo mengine,

ila utaweza tu kusoma taarifa zinazohitajika kutoka kwenye mifumo mengine ili kulinda usalama wa taarifa zake.

Mfumo wa watumishi wa Umma utasaidia kupata taarifa za viongozi punde tu watakapoteuliwa na kuingizwa kwenye mifumo, hivyo kurahisisha upatikanaji wa taarifa sahihi za viongozi kama vile nafasi zao za kazi, vyeo, taarifa za mishahara na maposho, na kuepusha kuingizwa kwa taarifa zenye utofauti na zile zilizopo kwenye mifumo mengine. Aidha, Mfumo wa vitambulisho utasaidia katika kuhakikisha kwamba kitambulisho cha kiongozi kilichowekwa katika mfumo ni sahihi na kitasaidia katika kupata taarifa kama vile picha, tarehe ya kuzaliwa na taarifa nyingine muhimu zitakazokua zinahitajika kwa wakati huo.

## 5.4 UPOKEAJI NA UCHUNGUZI WA TUHUMA NA MALALAMIKO YA UKIUKWAJI WA SHERIA YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

Katika kipindi cha mwaka 2021/2022, Tume ilipokea na kuyafanyia kazi jumla ya malalamiko 22 ya ukiukwaji wa Maadili ya Viongozi sawa na asilimia 110. Idadi hiyo ni ongezeko wa malalamiko 2 ikilinganishwa na malalamiko 20 yaliyopangwa kupokelewa katika kipindi hiki cha utekelezaji. Hali hii inawezekana kuwa imechangiwa na ongezeko la utoaji elimu kwa Wananchi kupitia Shehia, Vijana kupitia Mabaraza ya Vijana Wilaya, Wanafunzi kupitia Skuli, Wasanii kupitia Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni na wananchi kwa ujumla kupitia vyombo vya Habari ikiwemo televisheni na redio. Maeneo ambayo malalamiko hayo yalijikita ni pamoja na matumizi mabaya ya madaraka (18), udhalilishaji wa kijinsia (2), upendeleo katika ajira (1) na kutelekeza familia (1). Malalamiko hayo yako katika hatua tofauti za kufanyiwa kazi kama zinavyojieleza ***Jadweli Nambari 5 na 6.***

**Jadweli Nambari 5: Idadi ya Malalamiko yaliyopokelewa hadi 2021/2022**

| S/N | Malalamiko | 2016/17 | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Malalamiko yaliyopokelewa na kufanyiwa kazi na Tume | 3 | 6 | 10 | 17 | 10 | 20 |
| 2 | Malalamiko yaliyopokelewa na kupelekwa Taasisi nyengine | 1 | 0 | 3 | 3 | 2 | 2 |
| | **Jumla ya Malalamiko yaliopokelewa** | **4** | **6** | **13** | **20** | **12** | **22** |

## 5.4.1 Uchambuzi wa Malalamiko

Malalamiko kumi na nane (18) kati ya ishirini na mbili (22) yanahusiana na matumizi mabaya ya madaraka. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko kumi (10) yametolewa maamuzi, malalamiko matano uchunguzi wake unaendelea na malalamiko matatu uchunguzi wake umekamilika na wahusika wanasubiri kuitwa mbele ya Tume kwa ajili ya kusikilizwa utetezi wao.

Kwa upande mwengine, malalamiko mawili (2) kati ya 22 yanahusiana na udhalilishaji wa kijinsia ambapo moja kati ya hayo uchunguzi wake bado unaendelea na lalamiko moja uchunguzi wake umekamilika na wahusika wanasubiri kuitwa mbele ya Tume kwa ajili ya kusikilizwa utetezi wao.
Kadhalika, malalamiko mawili (2) kati ya 22 yaliyobakia, moja linahusiana na upendeleo katika ajira na moja linahusiana na kutelekeza familia ambapo yote tayari yametolewa maamuzi. Malalamiko hayo yaliyowasilishwa Tume yamehusisha watendaji wakuu wa Wizara, Idara na Taasisi za SMZ wakiwemo baadhi ya Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, Wakuu wa Mikoa na Wilaya na Wakuu wa Taasisi za Umma.

Aidha, Tume kupitia programu zake za utoaji wa elimu itaendelea kutoa elimu kwa viongozi na watumishi wa umma ili kuzidi kuelelewa na kufuata masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa lengo la kuhakikisha kuwa viongozi wanafuata maadili ya utumishi wa umma katika utekelezaji wa majukumu yao kwa umma.

**Jadweli Nambari 6: Uchambuzi wa Malalamiko yaliyopokelewa hadi 2021/2022**

| SN | Aina ya Malalamiko | Idadi | Hatua | Hali halisi |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Matumizi mabaya ya madaraka | 18 | Maelezo yamechukuliwa Vielelezo vimekusanywa | Uamuzi umetolewa (10)<br>Uchunguzi umekamilika (3)<br>Uchunguzi unaendelea (5) |
| 2 | Udhalilishaji wa kijinsia | 2 | Maelezo yamechukuliwa Vielelezo vimekusanywa | Uchunguzi umekamilika (1)<br>Uchunguzi unaendelea (1) |
| 3 | Upendeleo katika ajira | 1 | Maelezo yamechukuliwa Vielelezo vimekusanywa | Uamuzi umetolewa (1) |
| 4 | Kutelekeza familia | 1 | Maelezo yamechukuliwa Vielelezo vimekusanywa | Uamuzi umetolewa (1) |
| | **Jumla ya Malalamiko** | **22** | | |

## 5.5 KUJENGA UELEWA KWA WANANCHI NA VIONGOZI WA UMMA UNGUJA NA PEMBA KUHUSU MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

Kwa mujibu wa kifungu cha 12(1)k cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, utoaji wa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa maadili ni moja kati ya majukumu ya msingi ya Tume ya Maadili. Jukumu hilo limetekelezwa kwa kutumia njia na mbinu mbalimbali ikiwemo mikutano ya viongozi wa umma na wananchi, vipindi vya redio na televisheni, matangazo pamoja na Maadhimisho ya Siku ya Maadili.

### 5.5.1 Mikutano na Viongozi wa Umma na Wananchi

Katika kipindi hiki cha utekelezaji mwaka 2021/2022 Tume ya Maadili ilifanya jumla ya mikutano ya utoaji elimu 75 kwa viongozi wa umma na wananchi. Kati ya mikutano hiyo, mikutano 25 ilifanyika katika Wizara na Taasisi zake kwa viongozi na watendaji wake, mikutano 11 ilifanyika Wilaya zote kwa madiwani na masheha Unguja na Pemba.

Aidha, mikutano 39 ilifanyika kwa wananchi wa makundi tofauti, ambapo Shehia mikutano 15, Skuli za Sekondari mikutano 16, Mabaraza ya Vijana mikutano 7 katika Wilaya zote za Unguja na mkutano mmoja ulifanyika kwa Wasanii wa Mikoa mitatu ya Unguja.  Katika mikutano hiyo, mada kuu zilizowasilishwa na kujadiliwa katika mikutano hiyo ni pamoja na Umuhimu wa Kuimarisha Maadili katika Jamii, Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 4 ya 2015, Ujazaji wa Fomu (mpya) ya Tamko la Rasilimali na Madeni kwa Viongozi wa Umma na Wajibu wa Wananchi (Shehia, Wanafunzi, Vijana na Wasanii) katika kuisaidia Tume kutekeleza majukumu yake ***Jadweli Nambari 7, 8 na 9 yanahusika.*** Kadhalika, jumla ya vipeperushi 3,520 viliandaliwa, kuchapishwa na kusambazwa kwa viongozi na wananchi kupitia mikutano hiyo.

**Jadweli Nambari 7: Orodha ya Shehia na Wananchi wake Zilizopatiwa Elimu ya Maadili**

| Na. | JINA LA SHEHIA | IDADI YA WATU |
|---|---|---|
| 1 | MPENDAE | 93 |
| 2 | MWEMBE MAKUMBI | 117 |
| 3 | MKOKOTONI | 34 |
| 4 | MWANDA | 18 |
| 5 | FUJONI | 195 |
| 6 | KISONGONI | 85 |
| 7 | MFENESINI | 128 |
| 8 | MBUZINI | 59 |
| 9 | NUNGWI KIUNGANI | 83 |
| 10 | MARUMBI | 41 |
| 11 | UMBUJI | 38 |
| 12 | KZ/MKUNGUNI | 50 |
| 13 | DONGWE | 102 |
| 14 | KINUNI | 145 |
| 15 | FUMBA | 26 |
| | **JUMLA** | **1,214** |

**Jadweli Nambari 8: Orodha ya Skuli na Wanafunzi Zilizopatiwa Elimu ya Maadili**

| NA | JINA LA SKULI | IDADI YA WANAFUNZI |
|---|---|---|
| 1 | MGAMBO | 79 |
| 2 | PALE | 112 |
| 3 | K/SAMAKI "B" | 65 |
| 4 | FARAJA | 401 |
| 5 | KIWENGWA | 114 |
| 6 | DONGE | 132 |
| 7 | MWENGE | 136 |
| 8 | M/KWEREKWE"C" | 363 |
| 9 | CHWAKA | 111 |
| 10 | CHUINI | 252 |
| 11 | CHUMBUNI | 204 |
| 12 | MAKOBA | 261 |
| 13 | PAJE | 164 |
| 14 | KITOGANI | 150 |
| 15 | MATEMWE | 47 |
| 16 | DUNGA | 92 |
| | **JUMLA** | **2,683** |

**Jadweli Nambari 9: Orodha ya Mabaraza na Vijana Yaliyopatiwa Elimu ya Maadili**

| NA | BARAZA LA VIJANA | IDADI YA VIJANA |
|---|---|---|
| 1 | WILAYA YA KUSINI | 13 |
| 2 | WILAYA YA KATI | 55 |
| 3 | WILYA YA KASKAZINI “A” | 35 |
| 4 | WILAYA YA KASKAZINI “B” | 50 |
| 5 | WILAYA YA MAGHARIBI “A” | 27 |
| 6 | WILAYA YA MAGHARIBI “B” | 45 |
| 7 | WILAYA YA MJINI | 44 |
| | **JUMLA** | **269** |

### 5.5.2 Utayarishaji na Urushaji wa Vipindi vya Elimu na Matangazo kupitia Vyombo vya Habari

Katika kipindi hiki cha utekelezaji kwa mwaka 2021/2022, Tume ya Maadili iliandaa na kurusha hewani jumla ya vipindi 12 vya elimu kwa umma kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) – Redio (4) na Televisheni (4) na kupitia vyombo vya habari binafsi ikiwemo Zanzibar Cable vipindi 2, Radio Jamii Tumbatu kipindi 1 na Redio Hits FM kipindi 1. Katika vipindi hivyo, mada kuu iliyozungumzwa ni Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na umuhimu wa kuimarisha maadili. Mbali na mada hiyo mambo mbalimbali yanayohusiana na utekelezaji wa Sheria hiyo yaliyojadiliwa na kutolewa ufafanuzi.

### 5.5.3 Utayarishaji na Utoaji wa Matangazo

Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeweka muda maalum wa uwasilishaji wa Fomu za Tamko la Mali na Madeni. Tume ya Maadili ilifanikiwa kutayarisha na kutoa matangazo mbalimbali kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) - Redio na Televisheni kwa lengo la kuwakumbusha na kuwahimiza Viongozi wajibu wao na kutekeleza masharti yaliyomo katika Sheria ya Maadili ikiwa ni pamoja na kuwasilisha Fomu ndani ya muda uliowekwa kisheria.

Matangazo hayo yalirushwa na kusikika katika kipindi chote cha mwezi wa Disemba, 2021 kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) - Redio na Televisheni.

### 5.5.4 Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu

Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu ni njia nyengine muhimu inayotumika kuelimisha viongozi wa umma na wananchi. Lengo na madhumuni ya kufanyika maadhimisho hayo ni kukuza na kuongeza uelewa wa viongozi na wananchi juu ya dhana ya Utawala Bora na misingi yake. Misingi hiyo ni pamoja na masuala ya mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu wa uchumi, usimamizi wa rasilimali za umma, kuheshimu Haki za Binadamu, uwajibikaji, uwazi na uadilifu. Maadhimisho hayo yalifanyika tarehe 13 Disemba, 2021 kwa mafanikio makubwa katika Ukumbi wa Sheikh Idriss Adul Wakili Kikwajuni Unguja, ambapo Viongozi wa Umma na wananchi walihudhuria. Mgeni Rasmi katika kilele cha sherehe ya maadhimisho hayo alikuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Maadhimisho hayo yaliandaliwa kwa ushirikiano kati ya taasisi zinazohusika na masuala ya Utawala Bora. Taasisi hizo ni Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Idara ya Utawala Bora na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Kauli mbiu ya Maadhimisho hayo kwa mwaka 2020 ni “Piga vita Rushwa, Heshimu Haki za Binadamu, Uadilifu na Uwajibikaji kwa Maendeleo ya Uchumi Endelevu”.

## 5.6 MAFUNZO YA KITAALAM KWA WATUMISHI WA TUME YA MAADILI

Tume ya Maadili katika kuwajengea uwezo watumishi wake imefanikiwa kuwapatia mafunzo maalum ya ndani yanayohusiana na matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili wa Taarifa za Viongozi wa Umma, mafunzo juu ya dhana nzima ya maadili na uchunguzi pamoja na mafunzo yanayohusiana na Kukabiliana na Majanga ya Moto yaliyotolewa na Kikosi Cha Zimamoto na Uokozi. Watumishi wote wa Tume walishiriki mafunzo hayo kwa lengo la kuleta tija na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Tume. Kadhalika, mfanyakazi mmoja anaendelea kusomeshwa mafunzo ya muda mrefu katika fani ya Sheria na mfanyakazi mmoja amehitimu masomo yake ya Shahada ya Kwanza katika fani ya Uongozi.

## 5.7 KUANDAA NA KUWASILISHA RIPOTI YA MWAKA YA KAZI ZA TUME YA MAADILI

Kwa mujibu wa Kifungu cha 29(1) na (2) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya 2015, Tume ya Maadili inatakiwa kutayarisha Ripoti ya Mwaka ya Utekelezaji wa Kazi za Tume kwa kila mwaka na kuiwasilisha kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ndani ya miezi mitatu baada ya kumalizika mwaka wa fedha husika. Katika kipindi cha Utekelezaji kwa mwaka 2020/2021, Tume ilifanikiwa kuandaa Ripoti ya Tano ya Utekelezaji wa Kazi za Tume kwa Mwaka 2020/2021 na kuiwasilisha kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi tarehe 28 Septemba, 2021. Aidha, Ripoti hiyo iliwasilishwa na kujadiliwa mbele ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika Mkutano uliofanyika tarehe 15 Disemba, 2021.

## 6.0 VIKAO VYA TUME YA MAADILI

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya vikao kumi vya Tume vilifanyika, ambapo mambo mbalimbali kuhusiana na masuala ya Tume ya Maadili na ya Viongozi wa Umma yalijadiliwa na kutolewa uamuzi. Miongoni mwa mambo yaliyojadiliwa ni Ripoti ya Utekelezaji wa Kazi za Tume kwa Mwaka 2020/2021; Orodha ya Majina ya Viongozi waliowasilisha Fomu ya Tamko la Mali na Madeni kwa mwaka 2021/2022 na kuchapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali kupitia Tangazo la Kisheria Nambari 39 na 101 la mwaka 2022; Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Maadili (Miezi 9) kwa mwaka 2021/2022 na Mwelekeo wa Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2022/2023.

Kadhalika, vikao vya Tume pia vilihusisha usikilizaji wa malalamiko ya wananchi kuhusu ukiukwaji wa maadili ya viongozi wa umma.

### 6.1 KUSILIKIZA NA KUTOA MAAMUZI KUHUSU MALALAMIKO YA UVUNJAJI WA MAADILI YA VIONGOZI

Miongoni mwa jukumu la msingi la Tume ni kupokea na kusikiliza malalamiko na madai ya uvunjwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma dhidi ya Viongozi wa Umma (kifungu cha 23(1)(2)(3) cha Sheria ya Maadili). Katika kipindi hiki cha utekelezaji 2021/2022, Tume ilisikiliza malalamiko 8 yanayohusiana na uvunjwaji wa Sheria ya Maadili dhidi viongozi wa umma. Viongozi waliohusika walitakiwa kutoa maelezo yao kwa maandishi kuhusiana na tuhuma zinazowakabili na walipewa fursa ya kufika mbele ya Tume na kupewa haki ya kusikilizwa na Tume. Kwa upande wa viongozi ambao Tume iliwaona kuwa wamevunja maadili ya viongozi kinyume na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma,

Ripoti na Maamuzi ya Tume yaliwasilishwa kwenye mamlaka za uteuzi wa viongozi hao kwa ajili ya hatua za kinidhamu, kama Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma inavyoelekeza.

## 7.0 HALI YA MAPATO NA MATUMIZI

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Tume iliidhinishiwa jumla ya Tshs. 1,152,100,000 ambapo Tshs. 855,100,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo na Tshs. 297,000,000 kwa ajili ya kulipia mishahara na stahiki za watumishi. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022, jumla ya Tshs. 333,000,000 sawa na asilimia 39 zilipatikana kwa ajili ya matumizi mengineyo na Tsh. 206,258,057 zilipatikana kwa ajili ya kulipia mishahara na stahiki za watumishi.

Muhtasari wa hali ya mapato na matumizi ni kama unavyoonekana katika ***Jadweli Nambari 10*** linahusika.

**Jadweli Nambari 10: Hali ya Mapato na Matumizi.**

| MWAKA | RUZUKU | KILICHOTENGWA | KILICHOPATIKANA | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| **2017/2018** | Mshahara na Stahiki | 116,660,000 | 116,660,000 | 100 |
| | Matumizi Mengineyo (OC) | 500,000,000 | 415,000,000 | 83 |
| | **Jumla** | **616,660,000** | **531,660,000** | **86** |
| **2018/2019** | Mshahara na Stahiki | 212,400,000 | 212,400,000 | 100 |
| | Matumizi Mengineyo (OC) | 525,000,000 | 490,000,000 | 93 |
| | **Jumla** | **737,400,000** | **702,400,000** | **95** |
| **2019/2020** | Mshahara na Stahiki | 296,372,160 | 289,540,415 | 98 |
| | Matumizi Mengineyo (OC) | 681,500,000 | 519,098,885 | 76 |
| | **Jumla** | **977,872,680** | **808,639,300** | **83** |
| | **Maendeleo** | **50,000,000** | **50,000,000** | **100** |
| **2020/2021** | Mshahara na Stahiki | 296,372,160 | 292,161,502 | 99 |
| | Matumizi Mengineyo (OC) | 788,300,000 | 187,183,706 | 24 |
| | **Jumla** | **1,084,672,160** | **479,345,208** | **47** |
| | **Maendeleo** | **175,000,000** | **78,175,925** | **45** |
| **2021/2022** | Mshahara na Stahiki | 297,000,000 | 206,258,057 | **69** |
| | Matumizi Mengineyo (OC) | 855,100,000 | 333,000,000 | **39** |
| | **Jumla** | **1,152,100,000** | **539,258,057** | **47** |

## 8.0 CHANGAMOTO NA UTATUZI WAKE

Tume ya Maadili imeendelea kupiga hatua na kupata mafanikio ya kuridhisha katika utekelezaji wa majukumu yake. Mafanikio hayo yanatokana na mipango na mikakati madhubuti iliyojipangia na inayosimamiwa vyema na

watendaji wa Tume. Licha ya mafanikio hayo, bado kuna changamoto mbalimbali ambazo zinaathiri utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili ipasavyo. Zifuatazo ni baadhi ya changamoto na njia zilizotumika kutatua changamoto hizo:

i. Uhaba wa watumishi wa Tume ya Maadili hasa katika fani/kada za Sheria na Uchunguzi - Tume itaendelea kuchukua hatua za kuongeza watumishi wenye sifa zinazohitajika na kuwapatia mafunzo ya kukuza uwezo watumishi wake; na

ii. Upungufu wa baadhi ya vitendea kazi na vifaa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Tume ikiwemo jukumu la utoaji wa elimu kwa wananchi, uchunguzi, usajili na uhakiki wa taarifa za viongozi. Vitendea kazi na vifaa hivyo ni pamoja na gari, kompyuta, vifaa vya usikilizaji wa mashauri ya malalamiko, n.k – Tume inaendelea na hatua za upatikanaji wa vitendea kazi na vifaa hivyo kupita bajeti yake ya mwaka 2022/2023.

## 9.0 MIKAKATI YA TUME YA MAADILI KWA MWAKA 2022/2023

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Tume ya Maadili imepanga kutekeleza mikakati ifuatayo:

i. Kuendelea kuimarisha Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili wa Taarifa za Mali na Madeni ya Viongozi kwa kuingiza taarifa za Viongozi katika Mfumo huo;

ii. Kuhakiki Taarifa za Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma Unguja, Pemba na Tanzania Bara;

iii. Kujenga uwezo wa Tume kwa kuongeza vitendea kazi, idadi ya watumishi na kuwapatia mafunzo yanayohitajika;

iv. Kuandaa na kutekeleza programu maalum ya Utoaji wa elimu ya Maadili pamoja na kuwafikia na kuwashajihisha watumishi wa umma na wananchi kuwasilisha malalamiko ya ukiukwaji wa Sheria ya Maadili;

v. Kukamilisha mapitio ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Kanuni za Sheria ya Maadili;

vi. Kuandaa kanuni za mgongano wa maslahi kwa Viongozi wa Umma; na

vii. Kuimarisha Tovuti ya Tume ili iendane na wakati.

## 10.0 HITIMISHO

Mpangokazi wa Tume ya Maadili kwa mwaka 2021/2022 ndio nyenzo iliyotumika katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Tume. Kwa ujumla utekelezaji wa kazi za Tume umekuwa wa kuridhisha licha ya kukabiliwa na baadhi ya changamoto. Ripoti hii ya Sita ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili imeelezea hali halisi ya utekelezaji wa majukumu yake iliyojipangia kwa mwaka 2021/2022. Ni matarajio ya Tume ya Maadili kuwa ripoti hii itasaidia kuongeza uelewa na ufahamu kwa viongozi wa umma, wananchi, taasisi za serikali na zisizo za kiserikali kuhusu majukumu na utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili.

## 11.0 UWASILISHAJI WA RIPOTI

Ripoti hii inawasilishwa kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, **Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi,** kwa mujibu wa kifungu cha 29(1) na (2) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya 2015, leo tarehe **29 Septemba, 2022.**

Kwa heshima, naomba kuwasilisha.



**ASSAA A. RASHID**
**MWENYEKITI**
**TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA**
**ZANZIBAR.**

## Kiambatanisho Nambari 1: Muundo wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma

